BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

Kikao cha Ishirini – Tarehe 29 Novemba, 2014

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waziri wa Nchi, kwanza, tunaomba utuhalalishie siku hii. Toa hoja ya kuhalalisha kukaa siku ya leo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mhehimiwa Spika, Kikao hiki cha Bunge kilipangwa kukaa jana na kwa kawaida Siku ya Jumamosi huwa hatukutani, naomba Waheshimiwa Wabunge wakubali tutengue Kanuni yetu ili tuweze kufanya kikao siku ya leo ya Jumamosi mpaka tumalize kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya kutengua Kanuni kuruhusu Bunge lifanye kazi Siku ya Jumamosi ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, tutaendelea kufanya kazi mpaka tutakapomaliza kazi iliyobakia.

Waheshimiwa Wabunge, jana tuliacha kazi yetu bila kupeana maagizo tunafanya nini siku ya leo. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kusema kwamba, tulipofikia jana tulikuwa tunatafuta *wording* ambayo inafaa vile tunavyotaka. Sasa nina uhakika tumewaboa sana wananchi kwa kutusikiliza tunabishania maneno humu ndani ...

WAJUMBE FULANI: Aaaah!

SPIKA: Aah, niachieni Kiti! Hii tabia ya kutokusikiliza watu wanaposema nadhani siyo nzuri katika maisha ya kawaida ya binadamu. Katika maisha ya kawaida tu ya binadamu, hata kama yule anayesema labda hai-*make sense* kile anachokisema, huwa tunasikiliza. Kwa mila na desturi zetu za Kiswahili hivi ndivyo inavyokuwa. Kwa hiyo, ninasema hivi, sasa hivi naahirisha Bunge ili *Caucuses* zikakae. Tunaahirisha mpaka saa tano, naomba mkafanye *wording* inayostahili halafu tutakutana tena saa tano.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa tano.

(Saa 3.02 asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka saa 5.00 asubuhi)

(Saa 5.00 Bunge lilirudia)

HOJA ZA KAMATI

Taarifa Maalum ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* Kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalum Kuhusiana na Miamala Iliyofanyika Katika Akaunti ya Escrow ya Tegeta Pamoja na Umiliki wa Kampuni ya *IPTL*

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kama ulivyotoa taarifa ya kuahirisha Bunge asubuhi, ulikuwa na nia njema kwamba, Wabunge tutumie fursa zilizopo kwenye Kanuni ya kukaa kwenye Vyama, tulizungumze hili jambo. Nilielewa kwamba, nia yako unataka tuondoke na Maazimio ambayo yatatuunganisha kama Wabunge tukitoka kama Bunge moja bila mgawanyiko.

Kazi hiyo tunaendelea nayo na sisi kwenye *Caucus* yetu ya CCM tumekaa, kwa sababu tulikuwa tunatakiwa kufanya marekebisho ya baadhi ya Maazimio ambayo yalitolewa hapa Bungeni. Sasa kwa nia hiyo njema na sisi kama upande wa Serikali na Chama cha Mapinduzi, tunakuunga mkono kwamba, lazima tutoke Bunge moja na Maazimio ambayo yana maridhiano, yenye uhai, yanayokubalika ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, bado tunachapa na tunaomba tuendelee kufanya *consultation* kidogo, kwa hiyo, ninaomba utupe muda wa saa moja, tutakaporudi tutakuwa tumeshamaliza ku-*consult* wote kama Bunge kwa pamoja.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi amesema kwamba, *consultation* zinazoendelea ni za upande wa CCM, lakini anasema kwamba, tunataka kutoka kama Bunge moja; haiwezekani tukatoka kama Bunge moja kama *consultation* za kwenda kuweka msimamo wa CCM ili kuja kutumia wingi wa CCM kupitisha maamuzi ya CCM, ambayo kwa *spirit* ya jana, yanaonyesha kabisa kwenda kinyume na maoni ya wananchi na kinyume na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako ili hizi njama za kwenda kuweka msimamo wa *Caucus* ya CCM kuchakachua mapendekezo ya Kamati zisiwe ndiyo mapendekezo ya Bunge.

SPIKA: Naomba u-*clarify* Mheshimiwa Lukuvi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, nataka kusema ya uwazi, nafikiri Mheshimiwa Mnyika amewahisha shughuli.

Hapa tumeomba saa moja ili tuendelee na mashauriano. Nia ya mashauriano, najua sisi tunataka kushauriana wote kama Bunge, ndiyo maana nimesema nataka tutoke pamoja. Kwa hiyo, ungeturuhusu tutumie saa hii, siyo vizuri sana kuwaambia wananchi tunashauriana na Mheshimiwa Mnyika na kadhalika, lakini uturuhusu tupate hii saa moja, tushauriane kama Bunge nje ili tuweze kurudi kama wamoja na ndiyo maana yangu.

Kwa hiyo, nazungumza lugha ya Mnyika, lakini kwa lugha tofauti.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane, Kimataifa, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Kombo na Mheshimiwa Shekifu na Waheshimiwa Wabunge wote, naomba wote mkae.

Waheshimiwa Wabunge, Kimataifa ndiyo tunavyofanya, yaani mnaweza kubishana kuandika sentensi moja mpaka mkalala mkaamka na mkalala tena mpaka mkafikia mwafaka.

Sasa mimi naagiza Viongozi wa upande wa Upinzani na Viongozi wa Chama Tawala, wakakae pamoja mpaka saa kumi.

WAJUMBE FULANI: Aaah!

SPIKA: Saa kumi ni mbali?

MJUMBE FULANI: Mheshimiwa Spika, tunasafiri!

SPIKA: Niliwaambia jana, anayetaka ukongea na Spika kuna utaratibu, unasimama unaitwa. Mheshimiwa Zitto, tunabishania muda!

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Mheshimiwa Spika, saa kumi ni mbali sana. Upande wa Serikali umeomba saa moja ya *consultation.*

SPIKA: Saa moja tu mimi naona mashaka!

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Ni ndogo?

SPIKA: *Okay,* amependekeza saa moja.

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Basi tupendekeze saa mbili kwa ajili ya *consultation*.

Napendekeza *consultation* ya saa mbili na baada ya *consultation*…

SPIKA: Mheshimiwa Zitto endelea!

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu; Serikali imeomba saa moja, napendekeza tutoe saa mbili kwa ajili ya *consultation* na baada ya hapo turudi hapa tuendelee na kazi za Bunge.

SPIKA: Anayepinga hoja hii nani? Mheshimiwa Mbatia!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri.

SPIKA: Pendekezo ni saa mbili au moja.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nakubali.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukaenda hata zaidi ya hapo, unajua Kamati ndogo ikishafanya kazi yake vizuri na pande zote zikashauriana vizuri, wakija hapa, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Waziri tukija hapa tuwe kitu kimoja; lakini kwa misingi ya kwamba, kusiwepo na mivutano ya vuta nikuvute au tusitoe taswira yoyote sasa ya kichama. Hii Kamati ni Kamati

ya Bunge siyo ya Chama, kwa hiyo, sasa isionekane ni suala la Upinzani *vis-a-vis* Serikali au *vis-a-vis* Chama cha Mapinduzi. Wabunge wachache waende wakakae kwa *consultation*, waangalie vizuri hiyo *wording,* tukija hapa muda utakuwa mfupi zaidi wa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba, badala ya kusema *two hours,* ni afadhali tuje hapa tutumie muda mfupi zaidi, tuje hapa saa nane, *three hours. (Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, saa zenyewe wengine wanataka kwenda kula chakula.

Tunachokisema ndugu zangu, tuwe Bunge la kisasa, hatuwezi kuwa Bunge la kienyeji. Bunge la kisasa ni lile ambalo mkifika kama tulipofikia hapa, mna *consult* mpaka mnabishana hata namna ya kuandika; ndivyo inavyofanyika Duniani kote. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema hii ina faida yake, kwa sababu moja, achana na kusema mtu ana upande, hapana; Viongozi wachache wa pande zote mbili sijui wangapi, lakini wachache wakakae. Uzuri wa ku-*consult* ninyi mkutane tena na pande zenu kutoa taarifa mliyokubaliana ama humu ndani au mtoe madaraka ninyi wengine wote kwa hao watakaokutana, wakikubaliana walete hapa Bungeni.

Wakilibaniana hao, tukubaliane kwamba, wakifika hapa sisi tunawaunga mkono. Hao wachache wakikaa tunawaunga mkono.

Mheshimiwa Ole Sendeka!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana na mapendekezo yako mawili muhimu. Moja, hilo la saa ulilosema. Hili la pande zote kutoa watu ninakubali, lakini kwamba watakayoyaleta lazima tuyakubali moja kwa moja tusifanye hivyo, maana wanaweza wakaenda wakashindwana, hatimaye mambo yanakuja kuisha hapa mbele yako.

Ninachotaka kusema ambacho sioni tabu kubwa sana kwamba, kutakuwa na mvutano mkubwa, tuwateue tu waende. Kwa kuwa muda huo pia wa mchana watu wanaweza kwenda kula na kurudi hapa na kazi ikawa imekamilika vizuri, itakuwa ni jambo jema kuliko uingie halafu ukute mambo hayajakaa vizuri.

Kwa hiyo, naunga mkono hoja hiyo uliyosema saa kumi. Sasa kama ni saa kumi basi undeni Kamati za pande zote mbili.

SPIKA: Mheshimiwa Wenje! Tu-*move*, tusitumie muda mwingi kubishana.

MHE. EZEKIAH D. WENJE: Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sana, kwanza, niseme naunga mkono hoja yako kwamba, hili suala linahitajika watu wapewe muda wa kufanya *consultation,* tufanye maridhiano na makubaliano ili tutakaporudi hapa tutumie muda mchache.

Sasa mimi napendekeza kama ifuatavyo:-

Namba moja, ni kweli tunahitaji hiyo *consultation;* kwa hiyo, hiyo timu itaundwa. Sasa ukitoa muda mrefu kidogo, uzuri wake kwa pande zote ni kwamba, Kamati itaenda, watakaa huko watazungumza, watakayokubaliana na sisi kwenye *Caucus* tutapata fursa pia ya kuwa *briefed* kabla hatujarudi humu ndani. Huu ndiyo uzuri wa kutoa muda mpana kidogo, hiyo dhana ya saa kumi unayosema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja inayotutaka turudi saa kumi, muda mrefu upatikane *Caucus* ziwe *briefed.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ili niungwe mkono.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wajumbe, nataka turudi saa kumi, kwa sababu tusije nusu tumerudia, nusu tumerudia tena. Viongozi watakaokwenda kuzungumza, mimi sijui ni wangapi upande huu na wangapi upande ule; wale Viongozi wetu wakakae kwa lengo moja. Mimi nadhani *spirit* yenyewe tumeipata wote, wakati mwingine ni maneno tunashindwa namna ya kuyaweka sawa.

Jana nimejisemea wengine ni *bush lawyers* pamoja na mimi ni *bush lawyer*, eti wamekasirika wengine! Kwani mimi siyo *bush lawyer*? Mimi ni *bush lawyer, I am a bush lawyer, seriously! (Kicheko/Makofi)*

A bush lawyer ni mtu yule anayejitahidi kutoa ushauri wa kisheria wakati siyo mwanasheria kama mimi. Sasa mnakasirika nini? *I am one of the bush lawyers,* sasa ninyi mnakasirika nini? Mnafikiri ni matusi! *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, tumekubaliana turudi saa kumi.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na hoja yako, angalizo tu …

SPIKA: Kaa kwanza. Kuhusu utaratibu, unasimama halafu mimi nitakuita. Mheshimiwa Silinde!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, naungana na suala la kurudi saa kumi, lakini tulikuwa tunatoa tu angalizo kwamba, kwa sababu pamekuwa na tuhuma nyingi na Wabunge wengi wametuhumiwa, wale wote wenye tuhuma kama Mwanasheria Mkuu, akina Mheshimiwa Chenge na wengine, wasiwepo kwenye Kamati ya Mashauriano. Waende watu *neutral,* wenye uwezo wa kufikia kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hilo tu natoa kama angalizo. Ahante. *(Makofi)*

SPIKA: Sawa, nimekubali. Mimi pia nilikuwa ninafikiria hivyo.

Wenzetu waliokuwa na hoja, siyo Kamati yote ya Zitto, Zitto atachukua watu wake wachache washirikiane na Kamati hiyo. Mheshimiwa Zitto kwa sababu ni mwenye hoja *original.* Kwa hiyo, naomba hawa wakutane.

Tukichukua watano watano kila upande itakuwa *too little?* Mtaelewana wenyewe?

MBUNGE FULANI: Wanasema wataelewana wenyewe.

SPIKA: Wataelewana wenyewe.

Kwa hiyo, nawahoji muiamue hoja ya kwamba turudi saa kumi kuendelea na kazi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya kurudi saa 10.00 jioni kuwapa nafasi Viongozi wa pande mbili kukutana ilikubaliwa na Bunge)

(Saa 5.13 asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 alasiri)
(Saa 10.00 alasiri Bunge lilirudia)

HOJA YA KAMATI

Taarifa Maalum ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* Kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalum Kuhusiana na Miamala Iliyofanyika Katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta Pamoja na Umiliki wa Kampuni ya *IPTL*

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Mimi sijui Kamati ilikuwa inaongozwa na nani na taarifa zikoje! Upande wa *Caucus* ya huku ni nani alikuwa anaongoza? Mheshimiwa Jenista Mhagama!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, *Caucus* yetu kwa makubaliano ya pamoja na *Caucus* ya wenzetu na kwa usimamizi wa Bunge, ulituma wawakilishi kama sita, lakini mpaka sasa tunaambiwa bado kazi inaendelea hawajaimaliza. Kwa taarifa tulizoletewa sisi kwenye *Caucus* yetu, sijui upande wa wenzetu. Kwa hiyo, wawakilishi wetu wote hawapo ndani ya Ukumbi wa Bunge mpaka sasa. Sijajua upande wa wenzetu kama wawakilishi ambao wanatoka kwa upande wao wapo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Sisi tulipofuatilia majibu tuliyopata ni kwamba, shughuli bado inaendelea na wote kwa pamoja bado wanaendelea na mjadala kuona wanaweza kuja na kitu gani kwa pamoja ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti na sisi kwa upande wetu, tumejulishwa kwamba, bado majadiliano yanaendelea.

SPIKA: Ni jambo la afya kabisa, kazi yetu leo lazima tuimalize saa mbili kasorobo. Kwa hiyo basi, *in the spirit* ileile ya kuendelea kuzungumza, naahirisha sasa Kikao cha Bunge mpaka saa moja.

(Saa 10.03 alasiri Bunge lilisitishwa mpaka saa 1.00 usiku)

(Saa 1.00 jioni Bunge lilirudia)

HOJA YA KAMATI

Taarifa Maalum ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalum kuhusiana na miamala iliyofanyika katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta pamoja na umiliki wa Kampuni ya *IPTL*

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sheria!

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, jana tarehe 28 Novemba, 2014, niliwasilisha hoja kwa niaba ya Serikali, chini ya Kanuni ya 57 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, kuhusu Marekebisho ya Hoja ya Taarifa Maalumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalumu Kuhusiana na Miamala Iliyofanyika Katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta Pamoja na Umiliki wa Kampuni ya *IPTL*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mawelezo ya hoja yangu kujumuishwa katika Marekebisho ya Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, ninatoa hoja ya kuondoa Hoja hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 58 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea, *Chief Whip* upande wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nami pia hapo jana tarehe 28 Novemba, 2014, niliwasilisha hoja chini ya Kanuni ya 57 (1) na 58(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu, kuhusu Marekebisho ya Hoja ya Taarifa Maalumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalumu Kuhusiana na Miamala Iliyofanyika Katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta Pamoja na Umiliki wa Kampuni ya *IPTL*.

Kutokana na maelezo ya hoja yangu kujumuishwa katika Marekebisho ya Mapendekezo ya Kamati ya Hesabu za Serikali, ninaondoa hoja hiyo kwa Mujibu wa Kanuni ya 58(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, name ninaomba kutoa hoja.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 28 Novemba, 2014, niliwasilisha hoja chini ya Kanuni ya 57 (1) na 58(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2013, Kuhusu Marekebisho ya Hoja ya Taarifa Maalumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalumu Kuhusiana na Miamala iliyofanyika katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta Pamoja na Umiliki wa Kampuni ya *IPTL*.

Kutokana maelezo ya hoja yangu kujumuishwa katika Marekebisho ya Mapendekezo ya *PAC*, ninaondoa hoja hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 58(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

MHE. MHONGA SAID RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kabwe Zitto**!**

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1)(a), ili niweze kuondoa Maazimio yote kumi na mbili ya Kamati na kuingiza Maazimio mapya manane, pendekezo hili linatokana na Kikao cha pamoja kati ya Wajumbe wa Kamati ya *PAC,* Kambi ya Upinzani Bungeni na Kambi ya Chama Tawala, ambapo kwa pamoja tumekubaliana kuwa, Maazimio yote yaliyowasilishwa na Kamati na yale ya Serikali, hali kadhalika na yale ya Kambi ya Upinzani Bungeni, yaondolewe na Maazimio mapya yaweze kuletwa mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe …

SPIKA: Omba kutoa hoja.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa nini tunafanya hivi? Baada ya jana pande zote waliosema wanaomba kutoa hoja, waliwasilisha hoja ndani ya Bunge hili; kwa hiyo, hazikuwa mali zao isipokuwa mali Bunge. Kwa hiyo, leo wanapoamua kutoa ni lazima wakubali kuzitoa na sisi tukubali kuzitoa.

Mtakumbuka kwamba, jana tulienda tukafikia Maazimio mengi tu na tuliyaamua hapa, kwa hiyo, ni lazima hoja aliyoitoa Mheshimiwa Zitto tuiondoe sisi wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji kwa hoja zote; aliyoitoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sheria, aliyoisema Mheshimiwa Tundu Lissu, aliyoisema Mheshimiwa Mnyika pamoja na hii aliyoisema Mheshimiwa Zitto.

Sasa nitawahoji muamue kama hoja hizo ziondolewe.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya kuondoa hoja zilizowasilishwa jana Bungeni ilikubaliwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, tunakubaliana kwamba, hoja zote zilizoletwa kwa mujibu wa Kifungu cha 57(1)(3) zote zimeondolewa; kwa hiyo, ninamwita Mheshimiwa Zitto, awasilishe hoja mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zitto!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1)(a), ikisomwa pamoja na Fasili ya Tano, ninaomba kuleta Maazimio ya Bunge kuhusu Hoja ya Taarifa Maalumu ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi Maalumu Kuhusiana na Miamala iliyofanyika katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta pamoja na Umiliki wa Kampuni ya *IPTL*.

Kabla ya kuanza kuwasilisha Azimio hili, ninaomba nitambue Waheshimiwa Wabunge ambao walishiriki katika Kikao cha Maridhiano, ambacho kimepelekea Maazimio haya kuweza kuletwa mbele yako.

Wabunge hao Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mheshimiwa James Momose Cheyo, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Hamis Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu, Mheshimiwa Angellah Kairuki na mimi mwenyewe. *(Makofi)*

SPIKA: Ninasikia umemruka Mjumbe mmoja sijui ni nani?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, Kambi ya Chama cha Mapinduzi pia ilimpeleka Mheshimiwa George Simbachawene. Kwa heshima kubwa, ninaomba Mheshimiwa Mwenyekiti atambue uwepo wa Mheshimiwa George Simbachawene kwenye Kamati hiyo. *(Makofi)*

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nimesahau majina mawili; Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe na Mheshimiwa George Simbachawene.

Kwa kuwa Taarifa Maalumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi Maalumu wa Malipo Yaliyofanyika Katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), umeonyesha Herbinder Singh Seth wa *PAP,* James Rugemalila wa Kampuni ya *VIP,* Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Waziri wa Nishati na Madini, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania *(TANESCO),* imeonyesha walihusika kwa namna moja au nyingine na kufanikisha kufanyika kwa miamala haramu ya fedha za Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta, kwenda kwa makampuni ya *Pan African Power Solutions (PAP)* na *VIP Engineering* and *Marketing VIP*.

KWA KUWA kwa sababu ya kuhusika kwa watu hao na mialamala iliyofanyika katika Akaunti ya *Escrow* imeliingizia Taifa hasara ya mabilioni ya fedha za Umma, zinatokana kwa kutokulipwa kwa kodi mbalimbali za Serikali na kushindwa kwa *TANESCO* kukokotoa upya kiwango cha malipo cha gharama za uwekezaji (*capacity charges)* wa *IPTL;*

KWA KUWA mabilioni ya fedha yaliyotolewa kwenye Akaunti ya *Escrow* yametumika kuwapa kile kinachoonekana kuwa ni rushwa, baadhi ya Viongozi na Maafisa wa Serikali kama vile Mawaziri, Majaji, Wabunge, Wenyeviti wa Kamati za Bunge, Wakuu wa Taasisi za Umma, Viongozi wa Dini, Mwakili wa Kujitegemea na watu binafsi;

NA KWA KUWA vitendo vilivyofanywa na watu hawa vinaashiria uzembe na makosa mbalimbali ya jinai kama vile wizi, ubadhirifu, kutakatisha fedha haramu, matumizi mabaya ya madaraka, rushwa na kupokea mali ya wizi;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, TAKUKURU, Jeshi la Polisi na Vyombo vingine husika vya Ulinzi na Usalama, vichukue hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, dhidi ya watu wote waliotajwa na Taarifa Maalumu ya Kamati, kuhusika na vitendo vyote vya kijinai kuhusiana na Miamala ya Akaunti ya *Escrow*, na watu wengine watakaogundulika kufuatia uchunguzi mbalimbali unaoendelea kuhusika katika vitendo vya jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taarifa Maalumu ya Kamati imeonyesha jinsi ambavyo *TANESCO* imekuwa ikitumia mabilioni ya fedha kulipa gharama za umeme unaozalishwa na *IPTL,* na hivyo kuathiri hali ya kifedha ya Shirika hilo;

NA KWA KUWA Taarifa Maalumu ya Kamati inaonyesha kwamba, *TANESCO* itaendelea kulipa fedha nyingi kwa ajili ya gharama za umeme huo wa *IPTL;*

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kuichukua mitambo ya kufua umeme wa *IPTL* na kuimilikisha kwa *TANESCO* kwa mujibu wa Sheria za nchi. *(Makofi)*

KWA KUWA kwa miaka mingi mikataba mibovu ya kuzalisha umeme kati ya *TANESCO* na makampuni binafsi ya kufua umeme imeisababishia *TANESCO* hasara ya mabilioni ya fedha na hivyo kutishia uhai wake wa kifedha;

NA KWA KUWA Bunge limekwishaazimia kwamba, Serikali iwasilishe mikataba husika Bungeni au kwenye Kamati zake, kwa lengo la kutekeleza vyema wajibu wake wa kusimamia na kuishauri Serikali;

NA KWA KUWA Serikali haijatekeleza Azimio hilo la Bunge hadi sasa;

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze Azimio husika la Bunge mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Bunge la Bajeti la Mwaka 2015/2016, Serikali iwasilishe Taarifa ya Utekelezaji wa Mapitio ya Mikataba ya Umeme;

NA KWA KUWA vitendo vya wizi, ubadhirifu wa mali ya umma, hujuma ya uchumi na ufisadi vimeongeza, kushamiri na kushirikisha Viongozi wa Kisiasa na Mafisa wa Serikali pamoja na wafanyabiashara wakubwa;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Sheria iliyounda TAKUKURU, TAKUKURU inashughulikia vitendo vya aina zote za rushwa zikiwemo rushwa ndogo *(Petty Corruption)* na rushwa kubwa na ufisadi *(Grand Corruption)* na matumizi mabaya ya madaraka;

NA KWA KUWA kwa sababu ya majukumu yake mapana Kisheria, TAKUKURU inaelekea kuelemewa kupambana na kudhibiti vitendo vya rushwa kubwa, ufisadi na hujuma za uchumi zinazotishia uhai wa Taifa letu kiuchumi, kijamii na kisiasa;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba; Serikali iandae na kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria iliyounda TAKUKURU, kwa lengo la kuanzisha Taasisi mahususi itakayoshughulikia kupambana na kudhibidi vitendo vya rushwa kubwa, ufisadi na hujuma za uchumi zinazotishia uhai wa Taifa kiuchumi, kijamii na kisiasa. *(Makofi)*

KWA KUWA Taarifa Malumu ya Kamati imeonyesha kwamba katika watu waliotajwa kuhusika kwa namna moja au nyingine katika kashfa ya miamala ya Akaunti ya *Escrow*, wapo pia Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania;

KWA KUWA Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imeweka utaratibu mahususi wa kushughulikia nidhamu ya Majaji;

NA KWA KUWA utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji kwa mujibu wa Katiba unamtaka Rais kuunda Tume ya Uchunguzi ya Kijaji kuchunguza tuhuma za utovu wa maadili dhidi ya Majaji;

NA KWA KUWA utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji kwa mujibu wa Katiba unamruhusu Rais kumsimamisha kazi Jaji au Majaji husika wakati uchunguzi wa tuhuma dhidi yake unaendelea;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aunde Tume ya Kijaji ya Uchunguzi, kuchunguza tuhuma za utovu wa maadili dhidi ya Jaji Aloysius Mujulizi na Jaji Profesa Eudes Ruhangisa wa Mahakama Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

KWA KUWA Taarifa Maalumu ya Kamati imeonyesha kwamba Benki ya *Stanbic Tanzania Ltd.* ilishiriki kupokea na kutakatisha fedha zilizotolewa kwa njia haramu kutoka katika Akaunti ya *Escrow* na kupelekwa katika akaunti zilizofunguliwa na Kampuni ya *PAP* katika Benki hiyo;

NA KWA KUWA Taarifa Maalumu ya Kamati imeonyesha kwamba akaunti za *PAP* katika *Stanbic Bank Tanzania Ltd* zimekwishafungwa baada ya fedha zote zilizotolewa katika akaunti ya *Escrow* kumalizika;

NA KWA KUWA Taarifa Maalumu ya Kamati inaonyesha kwamba kuna uwezekano fedha zilizotolewa katika akaunti za *PAP* na *VIP* zilipelekwa katika Benki nyingine;

NA KWA KUWA vitendo vya *Stanbick Bank Tanzania Ltd* na benki nyingine kupokea na kutakatisha fedha zilizotolewa kwenye Akaunti ya *Escrow* ni vitendo vya jinai kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu;

HIVYO BASI, Bunge linaanzimia kwamba, mamlaka husika za kifedha na za kiuchunguzi kuitaja *Stanbic Bank Tanzania Ltd* na benki nyingine yoyote itakayogundulika kufuatia uchunguzi wa mamlaka za kiuchunguzi, kujihusisha na utakatishaji wa fedha zilizotolewa katika Akaunti ya *Escrow* kuwa ni Taasisi zenye shaka ya utakatishaji wa fedha haramu *(Institutions of Money Laundering Concern)*. *(Makofi)*

KWA KUWA vitendo vya kijinai vinavyohusishwa navyo Viongozi wa Umma na Maafisa wa ngazi za juu Serikalini vinakiuka pia Maadili ya Viongozi wa Umma na kuwanyima Viongozi na Maafisa hao uhalali wa kundelea kushikilia nafasi za mamlaka katika Uongozi wa Umma;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa *TANESCO* wawajibishwe kwa kuishauri Mamlaka ya uteuzi kutengua uteuzi wao. *(Makofi)*

KWA KUWA katika watu walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kashfa ya miamala ya Akaunti ya *Escrow* wapo pia Viongozi wa Kamati za Kudumu za Bunge kama vile Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa *TANESCO;*

NA KWA KUWA Bunge na/au Kamati zake za Kudumu zina uwezo na mamlaka kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge ya kuwawajibisha Viongozi hawa wa Kamati kwa kuwavua nyadhifa zao;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Kamati husika za Kudumu za Bunge zichukue hatua za haraka na kwa vyovyote vile kabla ya Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge, kuwavua nyadhifa zao kwenye Kamati husika za Kudumu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono, ninaomba muiamue. Mheshimiwa Freeman Mbowe, tunaanza kujadili.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Ninaomba Mheshimiwa ukae kidogo**.**

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuzungumza. Ninaomba nizungumze kwa heshima kubwa kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ambayo imetajwa mapema na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Mahesabu ya Serikali, imefanya kazi yake kwa siku nzima ya leo, imetafakari kwa mapana sana na kwa kina sana ni uamuzi Bunge hili lifanye ili kurudisha hali ya utulivu katika Taifa.

Wote tutakumbuka kwamba Kamati jana ilifanya mapendekezo mengine mengi tu, lakini kwa busara za Viongozi tuliokutana na baada ya kushauriana kwa kina, tulikubaliana Maazimio hayo manane yatoshe kufikisha ujumbe.

Mheshimiwa Spika, wote tutakumbuka kwamba, Kamati jana ilikuwa imefanya mapendekezo mengine mengi tu lakini kwa busara za Viongozi tuliokutana na baada ya kushauriana kwa kina tulikubaliana Maazimio hayo manane yatoshe kufikisha ujumbe kwa wote wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, sitapenda kuzungumza mengi sana katika hatua ya sasa, ila niombe tu sana, wenzetu ambao wapo katika Serikali, wao ndiyo ambao wana wajibu wa kwanza wa kulinda rasilimali za Taifa hili. Pale tunapokuwa wakali kujaribu kusukuma uwajibikaji katika Serikali, isichukuliwe kama ni chuki binafsi ama pengine ni wivu wa madaraka. Kwa hiyo, tuwaombe tu wanaohusika, watekeleze wajibu wao na watekeleze wajibu wao kwa uadilifu, wakitambua kwamba kuna Watanzania wengi ambao uaminifu wao na uadilifu wao, utawasaidia kuwaondoa katika lindi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, ninaomba kuunga mkono hoja hiyo. Kipekee sana nikimwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda, yeye kama Kiongozi Mkuu wa Serikali ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge, awe mkali zaidi, ili aisaidie Serikali, siku nyingine tusijikute katika mazingira ya mshike mshike dhidi ya Waziri Mkuu kama ambavyo safari hii ilikuwa. Tunakuomba Waziri Mkuu uwe mkali, uchukue hatua, usisubiri mpaka tufikie hatua ambayo tumefikia kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Filikunjombe.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niseme machache kwa niaba ya Kamati yetu ya *PAC*. Kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wote wa Kamati, tuliofanya kazi hii ya uchunguzi; Wajumbe wa Msingi pamoja na Wajumbe wengine watatu ambao tuliiomba ofisi yako waje watusaidie, nataka kulishukuru sana Bunge lako Tukufu; kwanza kabisa, kwa kuipokea Ripoti yetu ya *PAC*; pili, kwa kuijadili; na tatu, kwa kui-*adopt* humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzoni tulitaka kusononeka kwa sababu ya kuvutana. Sasa nataka wenzetu pia mwone kwamba, Kamati ya *PAC* tumefanya kazi hii kwa siku sita, tumekuja na matokeo hapa ndani, nataka mwone namna gani tulikuwa na changamoto ya kuchambua, kuchunguza na hatimaye kukubaliana kwenye mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwako, Kamati ya *PAC* ni Kamati yako, Kamati ya *PAC* ni Kamati yetu sisi Wabunge, Kamati ya *PAC* inapofanya kazi hatumwonei mtu, tunatenda haki kwa kila mmoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimshukuru kila mmoja kwa mchango wake. Tulifika mahala humu ndani Bungeni tukagawanyika kwa misingi ya Vyama. Tulianza kusababisha mpasuko bila sababu ya msingi. Nataka niseme kwamba, ninafurahi sana, kwa niaba ya wenzangu na kwa niaba ya Kamati, tumefika mahali tumeweka Vyama vyetu pembeni, tumeweka masilahi ya nchi, tumeweka masilahi ya Bunge letu na tumeshikamana pamoja. Ninamshukuru sana kila Mbunge, tumevutana, tumelumbana, tumesigana, lakini mimi ninaamini nia yetu ilikuwa ni moja kuwatetea, kuwapigania na kuwawakilisha wananchi wetu ambao wametutuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makosa kwenye baadhi ya maeneo ni kweli yamefanyika. Kwa niaba ya wenzangu, kwa niaba ya Kamati na kwa Ripoti hii, ninafurahi kuona hatua stahiki zitachukuliwa kwa kila mmoja aliyefanya uzembe kwa makusudi au kwa kutotimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Sisi kama Kamati tunapenda kusema hatutaweza kuliangusha Bunge lako na hatutaweza kuuangusha Mhimili wako. Ninataka niseme kwamba, tunaahidi kwa Watanzania na kwako mwenyewe kwamba, tutazidi kufanya kazi hii vizuri na kwa uaminifu zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati, napenda kukushukuru sana wewe mwenyewe binafsi. Napenda kuishukuru sana Ofisi ya Katibu wa Bunge. Napenda kumshukuru sana Dkt. Thomas Kashililah, ambaye tulikuwa tunakesha naye mara nyingine mpaka usiku kwenye kazi hii ya uchunguzi. Nawashukuru sana Makatibu wote, ile siku ya mwisho tulikesha mpaka saa kumi na mbili tukatawanyika. Kimsingi, tulikuwa tunalinda Ripoti yetu isiibiwe na pia mafisadi wasije wakaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru kila Mbunge, ninamshukuru kila mmoja na Wabunge wote pia kwa uvumilivu wenu. Napenda kusema ahsante sana, Mwenyezi Mungu awabariki sana. Mimi binafsi ninafurahi sana kwamba sasa hatua stahiki zitachukuliwa kwa kila mmoja kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Wasira!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nitumie muda mfupi sana katika kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, mimi nilikuwa miongoni mwa Wajumbe sita walioiwakilisha Serikali

na Chama cha Mapinduzi katika mjadala uliokuwepo. Tuliongozwa na Mheshimiwa Dada Anne Malecela katika kazi hii na yeye ndiye pamoja na wenzetu ndiyo wameniteua niseme kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mbowe, ambaye ni Kiongozi wa Upinzani, amekwishatoa taarifa juu ya kazi yetu. Mheshimiwa Deo Filikunjombe, alikuwa Mwenyekiti Mwenza, walikuwepo Wenyeviti wawili; Mheshimiwa Mama Malecela na Mheshimiwa Mbowe. Mwenyekiti Fulukunjombe amekwishatoa maelezo. *(Kicheko)*

SPIKA: Anaitwa Filikunjombe! *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nataka niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jana hali yetu ilikuwa mbaya sana, tulitoka hapa katika mazingira yasiyoeleweka na kwa sababu hiyo na kwa kuwa sisi ni Wawakilishi wa Wananchi, nina hakika na wananchi walikuwa katika hali mbaya vilevile; lakini palipo na binadamu hapaharibiki jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huo mtafaruku umetufundisha kwamba, tukikutana tukatumia busara, tunaweza kuamua jambo lolote ambalo linaonekana gumu na likawa rahisi. Tumekutana na tumejadiliana. Kazi yetu haikuwa rahisi, lakini tumejadiliana bila kugombana, tumebadilishana mawazo kwa uaminifu kabisa na kwa mapenzi makubwa, na kwa kweli tuliweka mbele masilahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, nataka kuwashukuru wenzetu wote kwa mjadala na kwa mapenzi makubwa ambayo yamekuwepo katika kufikia maafikiano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makubaliano yaliyosomwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, ndiyo makubaliano ambayo tumeyafikia na Chama cha Mapinduzi kimeshiriki kikamilifu katika kufikia makubaliano hayo. Tumeshiriki kwa sababu sisi tunaamini katika umoja, utulivu na maendeleo ya nchi hii; na kwamba jambo lolote linaloweza kuvunja umoja, kurudisha nyuma maendeleo na kuleta msukosuko katika nchi, haiwezi kuwa Sera ya CCM. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunafurahi kwamba tumefika hapo tulipofika na nataka wananchi wote waamini ya kwamba, Serikali ya CCM imeshirikiana na Kambi ya Upinzani katika kuleta makubaliano ambayo yataisaidia nchi yetu kwenda mbele. Kwa hiyo, tunaomba wananchi wayaunge mkono hayo tuliyokubaliana, lakini tunawaahidi kwamba, kwa upande wa Serikali, sisi tunao wajibu wa kutekeleza hayo ambayo yamesemwa. Kwa hiyo, tuna ziada ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, tunajua kwamba, mambo haya hayakuwa rahis,i yanagusa watu, wenzetu. Vilevile tujue ya kwamba, ukitazama masilahi mapana ya nchi, basi unakubali kwamba kuwajibika ni sehemu ya utekelezaji wa masilahi hayo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosoma Mheshimiwa Zitto, tumegusa kila Mhimili hata Bunge letu lenyewe, tumegusa Mahakama na tumegusa Serikali. Yote haya tumeyafanya kwa nia njema katika kuzingatia masilahi ya Watanzania na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Sawa nitawahoji muiamue hoja hiyo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika. Nina jambo la msingi.

SPIKA: Naomba ukae chini, Mheshimiwa Ole-Sendeka nimesimama, kwa hiyo, naomba ukae chini na uzime mashine.

(Maazimo Kuhusu Hoja ya Taarifa Maalum ya Kamati ya Hesabu za Serikali yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda, ninawapa hongera sana Kamati yangu yote iliyofanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukisema Bunge la wananchi maana yake ndiyo hiyo, kwa sababu tungetoka hapa ingekuwa wengine ni akina nani na nchi imegawanyika kama tulivyokuwa sisi humu ndani; ndiyo maana nikasema uvumulivu na tuchukue *International Standards*, mtazungumza weee mpaka mfike. Ninawashukuru sana, ninawapongeza sana na sipendi watu wachoke.

Mheshimiwa Ole- Sendeka, kuhusu mwongozo.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, niseme ili mamlaka yako…

SPIKA: Tuelewane, kifungu cha ngapi?

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7) na nilichotaka kuomba mwongozo baada ya Maazimio haya mazuri, hakuna eneo linaloeleza kwamba, taarifa zote zitakazofanyiwa kazi juu ya hoja hii, itatolewa taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa maana hiyo mkiacha Azimio likabaki hivyo, maana yake ni kwamba, ajenda hii hata mtakapookoa kiasi cha fedha mtakachookoa, mtakapoweza kuchukua hiyo mitambo kama mkiamua, mtakapokwenda kujua shilingi bilioni 73 zilizobebwa kwa malboro zimechukuliwa na nani, ni lazima taarifa ije hapa kwenye Bunge ili iweze kuendelea kujulikana; kwa sababu vinginevyo, ajenda hii utakuwa umeifunga na kwa kuifunga taarifa hii, maana yake itabidi uchukue miezi mingine kwa mujibu wa Kanuni ili uweze kuja kuifufua hoja hii upya.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninasema Azimio la aina hii ni muhimu liwekewe utaratibu utakaoripotiwa ndani ya Bunge lako Tukufu, na kwa maana hiyo naomba mwongozo wako kama utaniruhusu nitoe hoja juu ya hiyo ili taarifa hii iweze kuwasilishwa ndani ya Bunge hili kwa kadiri mafanikio itakavyowezekana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka, kitu kimoja nilichojifunza ndani ya Bunge hili ni kutokuaminiana kwa kila namna. Suala hili limetikisa nchi nzima. Sasa tutafika mahali tuseme tumefanya mchezo wa siku hizo basi tunaendelea hivyo hivyo. Kamati za Kisekta zipo, Kamati ya Uongozi ipo, Kamati ya Maadili ipo na watu wamewajibisha kundi kwa kundi nani anahusika hapo; mimi ninahusika na watu wa Kamati zangu zile.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuaminiane, tufanye kazi. Ninawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, kazi zilizopangwa katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba wa Bunge zimekamilika.

KUAHIRISHA BUNGE

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nataka nikuahidi kuwa, sitachafua hali ya hewa hata kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua umefanya kazi kubwa, lakini nataka nikuombe tu angalau nitumie dakika chache niseme mambo machache sana, kabla sijasema mawili, matatu, juu ya Maazimio tuliyoyapitisha sasa, kama ilivyo kawaida. Mengine yote leo nimeyasamehe, nimeona nijikite katika mambo yale ambayo ni ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha shughuli za Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba wa Bunge lako Tukufu na ni jambo la kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kutufikisha salama siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu ulijumuisha kujadili kazi kubwa zifuatazo; kwanza, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2015/16; pili, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi wa Mwaka 2014 (*The Tax Administration Bill, 2014);* tatu, Muswada wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 2014 *(The Value Added Tax Bill, 2014);* nne, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2014 *(The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2014);* na tano, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2014 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2014)*. Aidha, mapema leo Miswada mingine 11 ya Sheria za Serikali kuhusu mambo mbalimbali ilisomwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kushiriki katika Kamati ya Mipango hapa Bungeni, kwa kujadili kwa kina mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2015/2016. Maoni na ushauri tulioupokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge tutauzingatia wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Mwaka 2015/2016. Vilevile, ninawashukuru kwa kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria niliyoitaja hivi punde.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza Maswali ya Kawaida na yale ya Papo kwa Papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jumla ya maswali 241 ya msingi na maswali 662 ya nyongeza yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali 18 ya msingi na maswali 13 ya nyongeza yaliulizwa na kujibiwa kwa utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa, tarehe 17 Novemba, 2014 nilipata fursa ya kutoa kauli ya Serikali kuhusu migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji wa Wilaya ya Kiteto. Aidha, baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri walipata nafasi ya kutoa Kauli mbalimbali za Serikali kama ifuatavyo:-

Kwanza, Kauli ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu taarifa zilizotolewa na Vyombo vya Habari za kushutumu dhidi ya Serikali za China na Tanzania, kujihusisha na biashara haramu ya pembe za ndovu na ile inayohusu Kuridhia Mkataba wa

Umoja wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala wa Mwaka 2007. Pili, Kauli ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu hali ya dawa nchini na matibabu ya saratani nchini; Tatu, Kauli ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu mwenendo wa soko la nafaka na mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Novemba, 2014, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili na kupitisha Azimio la Bunge la kupongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Mbunge, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC PF)*. Aidha, katika Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge walipata pia fursa ya kujadili na kuridhia Maazimio mengine yafuatayo:-

(i) Azimio la Bunge kuhusu Itifaki ya kuanzishwa kwa Tume ya Utafiti wa Afya na Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(ii) Azimio la Bunge la kufuta na kusamehe madai au hasara itokanayo na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2011;

(iii) Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Ushirikiano katika masuala ya Kiulinzi *(The East African Protocol on Cooperation in Defense Affairs);*

(iv) Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Uzuiaji wa Vitendo haramu dhidi ya usalama wa Miundombinu ya Kudumu iliyojengwa chini ya Bahari katika Mwambao mwa Bara ya Mwaka 1988 *(The Protocol for the Suppression of Unlawful Acts Against the Safety of Fixed Platforms Located on the Continental Shelf)*.

Mheshimiwa Spika, Taarifa Maalum za Kamati: Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, Waheshimiwa Wabunge Walipokea Taarifa Maalum ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(Public Accounts Committee-PAC),* kuhusiana na miamala iliyofanyika katika Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta pamoja na umiliki wa Kampuni ya *Independent Power Tanzania Limited (IPTL)*.

Mheshimiwa Sika, naomba nitumie fursa hii, kwanza, kukushukuru wewe kwa kuruhusu Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC),* kuwasilisha Taarifa hii Maalum kwenye Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Aidha, nataka niwashukuru Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati, kwa uchambuzi wao wa kina na mapendekezo yao kama yalivyowasilishwa katika Mkutano huu.

Nitumie fursa hii kuwashukuru pia Waheshimiwa Mawaziri, waliozungumza kwa niaba ya Serikali nzima, kutoa maelezo yaliyolenga kutoa ufafanuzi wa hali halisi ya suala hili la Akaunti ya *Escrow* ya Tegeta na pia kujibu baadhi ya hoja za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitumie muda huu kuwahakikishia Wabunge na kuwaahidi Watanzania wote kwamba, kazi iliyo mbele yangu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali si Bungeni tu, lakini Serikali kwa ujumla, ni kuhakikisha kwamba, Maazimio yote ambayo yamepitishwa na Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yanasimamiwa na kutekelezwa kwa ukamilifu kama ilivyoshauriwa. *(Makofi)*

Ninataka niwatoe wasiwasi wanaofikiri kwamba pengine Serikali haitafanya jambo hili; hapana, tumeifanya kazi hii kwa nia njema na mimi nataka niwahakikishie tutahakikisha

tunatekeleza jukumu hili kikamilifu na tutawasilisha hapa Bungeni matokeo ya kazi hiyo tutakayokuwa tumeifanya. *(Makofi)*

La pili, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ilikuwa na hadidu za rejea 11. Katika hadidu hizo 11, yako mapendekezo mahususi yanayotakiwa kutekelezwa na Serikali 14. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, tumeshaunda Timu ya Wataalam, ambayo inapitia mapendekezo yote ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ili kuandaa majibu kwa kila eneo na baadhi ya majibu yatahusiana kwa karibu sana na Maazimio ambayo nayo yatatengenezewa utaratibu wa namna ya kuyatekeleza. Maazimio yote manane tutahakikisha yamefanyiwa kazi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja kati ya watu ninaoamini katika kauli isemayo; "Yaliyopita si ndwele sasa tugange yajayo." Nataka niungane na wenzangu waliosema kwamba, katika kujadili suala hili kumekuwepo na mambo mengi; kumekuwepo na kutiliana mashaka, katika maeneo mbalimbali; na kumekuwepo vilevile na lugha wakati mwingine kali; lakini zote hizi ilikuwa ni katika kuhitimisha jambo hili kwa masilahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, Serikali hii itaendelea kusimamia kwa nguvu zake zote kuhakikisha kwamba, mali na rasilimali za Taifa hili zinasimamiwa na kulindwa kikamilifu. *(Makofi)*

Katika zoezi hili na kama mlivyopendekeza katika Maazimio ambayo yamefanyika, wale wote watakaopatikana na ushahidi wa kutosha kuhusu mambo yoyote ambayo yatakuwa yamevunja Sheria za nchi hii, watashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria, watafikishwa kwenye Vyombo vya Sheria na Sheria itachukua mkondo wake. *(Makofi)*

Kwa wale ambao watalazimika kutumia taratibu za kiutawala, nataka niwahakikishie kwamba, hatua stahiki zitachukuliwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikalini wako wanaoniita mimi ni Mzee wa Bango Kitita. Kwa nini? Mara nyingi nimekuwa nikifanya kazi katika kutekeleza maagizo mbalimbali kwa kutumia mtindo wa kuhakikisha kwamba, kila lililoagizwa linatekelezwa na mtu ambaye ameainishwa na ndani ya muda ambao tumekubaliana. Kwa hiyo, Bango Kitita lile mara nyingi imekuwa ndiyo mwongozo katika ufuatiliaji. Hapa tutahakikisha kwamba, tunakuwa na Mabango Kitita kwa kila eneo ili kila mhusika aweze kutimiza wajibu wake inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko eneo moja ambalo naomba niliseme kwa nia njema tu na tutahakikisha kwa sababu ni moja ya jambo ambalo limeguswa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, nalo ni lile ambalo limeacha swali ambalo linatakiwa lijibiwe na litajibiwa kwa kazi mahususi. Je, fedha zilizoko katika *Escrow Account* ni za Umma? *CAG* kwa maana ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, ametuachia mwanya ambao lazima tuuzibe. Amesema inawezekana ipo fedha ya *TANESCO,* inawezekana ipo fedha ya *IPTL* na inawezekana ipo fedha ya serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa lugha hii maana yake nini kwa Serikali? Ni kwamba, ni lazima tuhakikishe tunafuatilia jambo hili kwa kina, tupate maelezo ya uhakika na tuje na maelezo kwenye Bunge lako Tukufu nini *reconciliation,* kwa maana ya kwamba hesabu zitakazokuwa zimefanyika, imeonyesha katika kujaribu kuondoa hili giza au ombwe ambalo limeachwa na swali hili muhimu sana. *(Makofi)*

Moja ambalo nataka nikubaliane kabisa na Wajumbe wa Kamati ambayo imefanya kazi nzuri sana ni lile la utekelezaji wa hukumu ya Mahakama, *ICSID II, ICSI* Namba Mbili, ambayo imetoa maelekezo kwa wahusika kukaa na kujaribu kutafuta ni namna gani tutaweza kufikia lile lengo la kubainisha kitu gani kimo katika *Escrow Account* na nani mwenye kitu gani, kwa kiasi gani. Kwa upande wa Serikali, tutashiriki kikamilifu kwa njia yoyote ile kuhakikisha kwamba, hili jambo na sisi tunashiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile niseme kwamba, jambo moja ambalo kwa Watanzania ni muhimu na lazima tuhakikishe linafanyika, linatokana na umuhimu wa kuteremsha bei ya umeme kwa ajili ya matumizi ya wananchi wetu. Ni kweli Mahakama ya kwanza ilitusaidia kiasi fulani kutoka dola milioni 3.6 hadi dola milioni 2.6. Mahakama katika umuzi huu wa pili, inaamini upo uwezekano mkubwa wa kushusha zaidi gharama hizo za umeme. Ndiyo maana nasema, kwa mtumiaji wa kawaida Mtanzania, zoezi hili ni lazima lifanyike na lifanyike kikamilifu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niseme kidogo juu ya suala hili ni lile linalohusiana na eneo la kodi ambazo zimo katika Taarifa hii ya *CAG,* lakini vile vile na Kamati ambayo Mheshimiwa Kabwe ameisimamia vizuri. Tunataka tuwahakikishie Wabunge na Watanzania wote, tutahakikisha kodi yote ambayo itabainika kwamba ni stahiki kwa ajili ya Serikali yetu inalipwa na kwa viwango vile ambavyo vitakuwa vimeainishwa. Jambo hili ni la msingi, kwa sababu fedha za umma lazima tuhakikishe kwamba inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee kuwashukuru sana sana Wajumbe wa Kamati na mimi nataka niseme kwamba, nilichojifunza leo mambo mengi kumbe yanawezekana. Mambo mengi kumbe yanawezekana, ulichokifanya leo ni kurejesha au kuturejesha katika utaratibu wa kitu kinaitwa Kamati ya Maridhiano. Kwa sababu tulikuwa na upande wa wenzetu, marafiki zetu Vyama vya Upinzani, upande wa Chama Tawala, tukashirikisha vilevile na *PAC* yenyewe, tumekaa pamoja, Maazimio yamepatikana tena ndani ya muda mfupi kuliko kama ambavyo tungekuwa tumehangaika kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nataka niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, huko tuendako, tunapokuwa na kazi nzito kama hizi, pengine jambo la busara ni kuona namna moja au nyingine, tuwe Kamati ya Maridhiano mapema ili tuweze kufikia mwafaka haraka zaidi na kuondoa mivutano ambayo haina msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. Nirejee kuwashukuruni sana Wabunge kwa kazi nzuri mliyoifanya kuhusiana na eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kueleza kidogo juu ya Serikali za Mitaa na Uchaguzi unaokuja.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara unatarajiwa kufanyika tarehe 14 Desemba, 2014. Uchaguzi huo ni wa kawaida na unahusisha Uchaguzi wa Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji, Mitaa, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji na Wajumbe wa Kamati za Mitaa. Taarifa nilizonazo ni kwamba, hadi sasa maandalizi ya msingi kuwezesha uchaguzi huo kufanyika yamekamilika. Ili kuhakikisha kuwa uchaguzi huo unafanikiwa, maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi yalifanyika kupitia Vikao vya wadau mbalimbali ili kupata maoni, mapendekezo na ushauri ambao umesaidia katika kuboresha Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Wadau walioshirikishwa ni pamoja na Viongozi wa Vyama vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Asasi Zisizo za Kiserikali.

NAKALA YA MTANDAONI

Mheshimiwa Spika, katika maandalizi ya awali, Orodha ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji iliandaliwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 22 Agosti, 2014, lenye Tangazo la Serikali Namba 300 kwa Halmashauri za Miji na Tangazo Namba 301 kwa Halmashauri za Wilaya. Orodha hiyo imejumuisha Kata, Vijiji na Mitaa. Katika uchaguzi wa mwaka huu jumla uya Vijiji 12,443, Vitongoji 64,616 na Mitaa 3,741 vitahusika kwenye uchaguzi. Naomba nirudie kidogo hapo; Orodha hiyo imejumuisha Kata, Vijiji na Mitaa na katika uchaguzi wa mwaka huu, jumla ya Vijiji 12,443, Vitongoji 64,616 na Mitaa 3,741 vitahusika kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha uchaguzi huo, Serikali imekwishaandaa na kuchapisha vipeperushi, fomu za wagombea, rejesta za wapiga kura, karatasi za kuonyesha vituo vya kupiga kura, mabango na matangazo mengine kuhusu elimu kwa mpiga kura. Tayari vifaa hivyo vimepekwa mikoani na vingine vinaendelea kupelekwa. Aidha, masanduku ya kupigia kura yameshanunuliwa na tayari yameshasambazwa katika mikoa yote Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wafuatilie kwa karibu zoezi hili na pale watakapobaini tatizo ambalo linastahili kufikishwa kwenye Ofisi yetu, wasisitize kufanya hivyo ili tuweze kuchukua hatua haraka za kusahihisha kasoro yoyote itakayokuwa imejitokeza. Kwa vile siku zilizobakia kufikia tarehe ya kupiga kura ni chache, natoa wito kwa wananchi ambao hawajajiandikisha, ooh ni siku ya leo, katika Rejesta ya Wapiga Kura, wafanye hivyo bila kukosa. Aidha, Viongozi wa Vyama vya Siasa wawahimize wanachama wao na wananchi kwa ujumla, wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kupiga kura. Aidha, Wasimamizi wa Uchaguzi wahakikishe vifaa vya uchaguzi vinafika kwenye maeneo yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa rai kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa, waendeshe kampeni kwa amani na kuepuka maneno ya uchochezi, kubaguana kwa misingi ya ukabila, rangi, udini ama hali ya mtu, mambo ambayo yanaweza kusababisha vurugu na uvunjifu wa amani. Aidha, naomba Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wanachama wao, wakishapiga kura wasiendelee kukaa katika vituo vya kupiga kura, bali watawanyike na kusubiri muda wa matokeo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; leo nimeona nizungumzie masuala muhimu tu tena machache sana. Kabla sijahitimisha, naomba basi nitumie nafasi hii, kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano. Kipekee, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Naibu Spika, kwa kutuongoza vizuri. Niwashukuru Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi nzuri ya kuongoza Vikao vya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya *PAC* na Kamati ya Maridhiano, ambayo imetuwezesha kukamilisha zoezi la *IPTL* kwa urafiki na udugu wa karibu. Vilevile niwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi nzuri na michango mbalimbali wakati wa Mkutano huu. *(Makofi)*

Naomba pia nimshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake wote, pamoja na Wataalam wote wa Serikali na Taasisi zake, ikijumuisha Taasisi ya Sekta Binafsi, kwa misaada ya Kitaalam na huduma mbalimbali za kufanikisha Mkutano huu. Niwashukuru pia Waandishi wa Habari, kwa kazi nzuri walizofanya kuhakikisha kuwa Taarifa za Majadiliano na maamuzi mbalimbali ya hapa Bungeni zinawafikia wananchi. Niwashukuru madreva kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuwasafirisha kwa usalama Waheshimiwa Wabunge, Viongozi mbalimbali, Wataalam na Wasaidizi wote walioshiriki katika Mkutano huu.

Nimalizie kwa kuwatakia wote safari njema mnaporejea kwenye maeneo yenu ya kazi na katika Majimbo yenu. Aidha, niwatakie mapumziko mema ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2015. Ninaamini kwamba, Mwenyezi Mungu atatulinda na kutuvusha salama sote kama tulivyo hadi kuuona Mwaka Mpya wa 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 27 Januari, 2015, Saa Tatu Asubuhi, litakapokutana katika Mkutano wa Kumi na Nane kwenye Ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maneno aliyosema.

Mimi pia ningependa kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge, tarehe 30 Desemba ndiyo siku ambayo tunapaswa kupeleka zile fomu za maadili.

Safari hii tumebadilisha utaratibu, fomu zitachukuliwa pale Ofisi ya Spika na kurudishwa Ofisi ya Spika, fomu mbili. Sasa waliorudisha hapa tunaondoka nazo, tumeshaandika kwenye *register,* wengine ambao hamjajaza msiende nyumbani kabla hamjajaza zile fomu. Zipelekeni hata kama mtapita Dar es Salaam basi pale kutakuwa na Ofisi. Wale ambao wanafikiri hawataenda Dar es Salaam, lazima mjaze kabla ya tarehe hiyo na nitashukuru kama mtazijaza sasa. Kwa sababu mwaka uliopita tulipata matatizo sana kwa wengine wenu hapa mnafahamu mpaka kupelekwa Mhakamani, ipo Mahakama kule. Kwa hiyo, hamna sababu ya kupata usumbufu huo. Mali zenyewe hamna sana, mnaweza kuzikumbuka. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, haiwezi kuwapa shida ya kujua ziko wapi. Hamuwezi kupata shida kujua ziko wapi. Madeni anayo Katibu hapa mnaweza kuomba mkajaza tu mle. Kwa hiyo, naomba mjaze. Safari hii tumebadilisha utaratibu, Tume itachukua kutoka kwangu. Kwa hiyo, mimi sasa nitawafuatilia mtu mmoja mmoja kabla ya tarehe 30 mtapigiwa simu wale ambao hamjaleta, tuondoe adha ya kuanza kutafutana basi inakuwa kama ni fujo. Kwa hiyo, wanaoweza kurudisha hapa Dodoma, watarudisha pale Ofisini kwangu. Watakaokuwa wanajazia Dar es Salaam warudishe pale Ofisini kwangu. Hakikisheni mnasaini kwenye *register* kama mmerudisha kwa tarehe inayohusika.

Naomba niwakumbushe hili ni suala muhimu sana kwenu. Baada ya kusema haya na mimi naona mmechoka sana sipendi kusema maneno mengi.

Kitu kimoja ambacho ninakiomba Wabunge, ni wajibu wetu sisi kwa niaba ya wananchi wote, kuhakikisha tunaisimamia Serikali vilivyo na kuhakikisha kwamba, tunafika mahali tunakuwa na mfumo wa Serikali ambao kila mtu anaweza kujivunia nao, lakini kazi hii inatakiwa ifanyike na sisi wenyewe. Kwa maana hiyo nimeshasema na ninarudia, watu wenye pesa zao wanaokuja kuwa-*lobby lobby* ninyi Wabunge jamani kataeni. *(Makofi)*

Narudia, sasa mbona mnapiga kelele! *I am very serious* kwa sababu kazi tunayotakiwa kufanya sisi *unless* sisi wenyewe ni safi hatuwezi kufanya kazi hiyo ya kusimamia Serikali. *(Makofi)*

Mtakapoendelea hata ninyi mtajikuta mko ndani. Nani amewaambia mna kinga? Hamna kinga! Kinga ya makosa ya jinai hata Wabunge hamnayo. Kwa hiyo na ninyi mtakapoendekeza mchezo huu, hakika mtajikuta mko ndani, hatutamwonea huruma mtu yeyote. *(Makofi)*

Matumaini na mategemeo na furaha ya Watanzania ni kwetu sisi. Kama chombo hiki kitaoza nani mwingine atakayewasimamia wananchi? *(Makofi)*

WAJUMBE FULANI: Hakuna!

SPIKA: Kwa hiyo, Kamati zangu nazo nitazisimamia na katika maeneo ya Kisekta pia itabidi muangalie maeneo ambayo hayako vizuri. Tutakuwa na timu nyingine hivi hivi lazima. Kwa sababu wananchi wategemee nini sasa? Kama hawatutegemei sisi wamtegemee nani?

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, *seriously* mtakuta mnawekwa ndani bila kueleweka. Ukishawekwa ndani na Ubunge wako umeishia hapo.

Waheshimiwa Wabunge, sina sababu ya kusema hivyo, naomba kabla sijawahoji tuimbe Wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Sasa nitawahoji kwamba Bunge hili liahirishwe sasa mpaka tarehe 27 Januari, 2015, Siku ya Jumanne, Saa Tatu Asubuhi hapa Domama. Sasa nitawahoji muiamue hoja hiyo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Kuahirisha Bunge ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waliosema ndiyo wameshinda. Wanaotaka kubakia humu ndani wameshinda pia.

Ahsante Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge hili mpaka tarehe 27 Januari, 2015.

(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 27 Januari, 2015 Saa Tatu Asubuhi)